

HALMASHAURI YA WILAYA YA TUNDURU
IDARA YA KILIMO, UMWAGILIAJI NA USHIRIKA



TAARIFA YA MAENDELEO YA KILIMO CHA
UMWAGILIAJI
KATIKA WILAYA YA TUNDURU

December, 2016

1.0 UTANGULIZI

1.1 Kilimo cha Umwagiliaji

Wilaya ya Tunduru ina fursa kubwa ya kuendesha na kuendeleza kilimo cha Umwagiliaji. Wilaya ya Tunduru ina kilomita za mraba 15,700 sawa na Hekta 1,570,000 zinazofaa kwa Kilimo, na kati ya hekta hizi, hekta 3,340 zinafaa kwa kilimo cha Umwagiliaji. Hata hivyo Hekta 1,281 tu sawa na asilimia 38.3 ya eneo lote linalofaa kwa umwagiliaji ni eneo linalotumika kwa umwagiliaji kwa sasa. Wilaya ina jumla ya skimu 13 za umwagiliaji, skimu 5 kati ya hizi ni skimu zinazoendelea kuboreshwa na skimu 8 bado hazijaboreshwa kama inavyoonekana kwenye jedwali hapa chini;

NA	JINA LA SKIMU	KIJIJI	KATA	ENEO (Hekta)		MAELEZO
				LINALOFAA KWA UMWAGILIAJI	LINALO MWAGILIWA KWA SASA	
1	CHINUNJE	CHINUNJE	MBESA	374	120	Haijaboreshwa
2	CHANGARAWWE	CHANGARAWWE	MATEMANGA	242	100	Haijaboreshwa
3	KITANDA	KITANDA	MLINGOTI MAGH	455	110	Inaendelea kuboreshwa (Banio na mfereji mkuu wa mita 2,950 umejengwa)
4	LEKINDO	LELOLELO	SISI KWA SISI	90	69	Inaendelea kuboreshwa (Banio na mfereji mkuu wa mita 2,400 umejengwa)
5	LEGEZAMWENDO	LEGEZAMWENDO	KIDODOMA	240	90	Inaendelea kuboreshwa
6	LUKUMBULE	LUKUMBULE	LUKUMBULE	241	87	Haijaboreshwa
7	MADABA	AZIMIO	MTINA	220	100	Inaendelea kuboreshwa (Mabanio 3 na mifereji mikuu imejengwa)
8	MISYAJE	MISYAJE	MARUMBA	280	120	Inaendelea kuboreshwa (Banio na mifereji mikuu yenye mita 3,300 imejengwa)
9	MKOTAMO	MKOTAMO	NAMASAKATA	422	115	Haijaboreshwa
10	MBATI	MBATI	MBATI	100	40	Haijaboreshwa
11	NAIKULA	NAIKULA	NAMASAKATA	215	120	Haijaboreshwa
12	NASYA	NASYA	TUWEMACHO	218	130	Haijaboreshwa
13	WENJE	WENJE	NALASI MAGH	243	80	Haijaboreshwa
JUMLA KUU				3,340	1,281	

Aidha, mipango ya Wilaya itaendelea kuziendeleza skimu kila inapopata fursa ya fedha za ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji.

1.2 Changamoto katika sekta ya umwagiliaji Wilayani Tunduru

Sekta ya Umwagiliaji inakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na;

- Fedha zinazotengwa kwa ajili ya ujenzi au ukarabati wa miundombinu ya Umwagiliaji ni kidogo kiasi cha kusababisha miradi kutokamilika kwa asilimia Mia moja.
- Wakulima kuwa wagumu kuchangia fedha taslimu au nguvu kazi wakati wa ujenzi au wakati wa Uendeshaji na Matunzo
- Wakulima kutotumia kanuni za Kilimo Bora cha Mpunga na mazao mengine.
- Uharibifu katika vyanzo vya maji na hivyo kupelekea upungufu wa maji kwa baadhi ya maeneo.
- Uhaba wa wakandarasi wenye uwezo na viwango vinavyotakiwa kulingana na mahitaji kwasababu ya ubovu wa miundombinu ya barabara na hii husababisha wakandarasi wengi kuogopa kuomba kazi.
- Wakulima kuwa wagumu kulima wakati wa kiangazi kwa kutumia miundombinu ya umwagiliaji kwani wakulima wengi bado wanategemea mvua za masika licha ya uwepo wa maji kipindi cha kiangazi ikiwa ndio lengo na dhana nzima ya Kilimo cha Umwagiliaji.
- Ukosefu wa barabara za shambani (Farm service roads) na zile za kuingilia (Farm Access Roads) unasababisha usafirishaji wa mazao yatokanayo na kilimo cha umwagiliaji kuwa mgumu.

1.3 Mikakati

Pamoja na changamoto za hapo juu, mikakati na jitihada za makusudi zimefanyika ili kukabiliana na changamoto tajwa hapo juu. Mikakati hiyo ni pamoja na;

- Kuendelea kutenga fedha za kutosha katika ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji.

- Kutoa mafunzo kwa wakulima wa Umwagiliaji juu ya Mwongozo kabambe wa Umwagiliaji (Comprehensive Guidelines) unaotoa mwongozo wa umuhimu wa wakulima kuchangia kuanzia hatua ya Uibuaji na Mipango, Ujenzi/Utekelezaji, Uendeshaji na Matunzo na dhana ya kulima kipindi chote cha mwaka bila kutegema mvua ambazo sasa hazitabiriki kutokana na mabadiliko ya tabia nchi.
- Kuendelea kutoa elimu kwa wakulima juu ya hifadhi bora ya vyanzo vya maji ikiwa ni pamoja na matumizi ya sheria ya hifadhi ya mazingira na Maji na kanuni bora za Kilimo hifadhi.
- Serikali sasa inaendelea na ujenzi wa barabara kuu za Namtumbo mpaka Tunduru na Tunduru mpaka Nanyumbu kwa kiwango cha lami na sasa ni matarajio yetu kuwa ushindani katika zabuni utakuwa mkubwa na hivyo uwezekano wa kupata wakandarasi wenye uwezo na sifa utakuwa mkubwa pia.
- Kuendelea kutoa elimu ya matumizi sahihi ya mbegu bora na pembejeo zingine za kilimo katika skimu za umwagiliaji.
- Halmashauri kupitia Programu ya Miundo Mbinu ya Masoko na Huduma za Kifedha Vijijini (MIVARF) imeshaanza na kazi za ujenzi wa barabara za kuingilia kwenye skimu nne ambazo zimeendelezwa. Jumla ya kilomita 22.9 za barabara zitajengwa kwa kiwango cha changarawe kwenye skimu za Misyaje, Madaba, Kitanda na Lekindo.

2.0 GHARAMA ZA UJENZI WA MIRADI ILIYOENDELEZWA

Gharama za ujenzi wa miradi 5 iliyoendelezwa, skimu za Kitanda, Misyaje, Legezamwendo, Madaba na Lekindo zinaonekana kwenye kiambatanisho 1.

Pamoja na salamu za kuendeleza kilimo cha Umwagiliaji, naomba kuwasilisha;

.....

CHIZA C. MARANDO

AFISA KILIMO, UMWAGILIAJI NA USHIRIKA (W)

TUNDURU